SWAHILI FORUM 14 (2007): 197-206

FASIHI SIMULIZI NA TEKNOLOJIA MPYA

STEVEN ELISAMIA MRIKARIA

Mtaalamu mmoja wa masuala ya mawasiliano Marshall McLuhan (2003) miaka zaidi ya hamsini iliyopita alisema ukweli kuhusu uelekeo wa dunia kuwa ndogo kila kukicha. Udogo huu unasababishwa na kuwa ya kisasa zaidi ambayo ndiyo imezaa dhana mpya na iliyochukua nafasi ya dhana nyingine. Dhana hii mpya napenda kuitaja kama teknolojia mpya, ambapo katika makala haya nitaichambua kama *fasihi simulizi na teknolojia mpya*.

Aidha katika makala haya nitaangalia kwa upande mmoja fikra na mawazo ya baadhi ya wanafasihi vikongwe tanabahisha na kuonyesha uwepo wa fasihi simulizi, halafu nitaangalia kwa undani fasihi katika uwanja wa teknolojia mpya, kisha nitaorodhesha athari zilizotokea katika jamii baada ya kuingia kwa teknolojia hii na mwisho nitatoa hitimisho la nini cha kufanya ili kukabili upotofu huu utamaduni, mila na desturi zetu.

Over 50 years ago, Marshall McLuhan (2003), a specialist in communication issues, said that the world is becoming smaller and smaller every starting day, a result of the emergence of modern communication around the world. This situation has given birth to the concept 'new technology'.

This article will break down this new concept by looking at it through the lens of oral literature, which is used in Swahili communities. However, oral Swahili literature uses Kiswahili language, which the language of communication at different levels throughout East and Central Africa.

The article will examine the ideals and opinions connected to oral literature described in the existing academic literature, and as one of the genres of narrative literature. It will look at the way in which the concept of new technology is explained by specialists, and in which ways this connects to oral literature. Advantages and effects which came about in the society after the coming of this notion will be discussed. The article ends with a conclusion and possible recommendations.

1. Utangulizi

Tunapoongelea juu ya fasihi simulizi na teknolojia mpya mara moja katika mawazo yetu panatokea wazo la fasihi simulizi ya kileo. Aidha kwa upande wa baadhi ya wanafasihi vikongwe panaibuka fikra na mawazo yenye kuonyesha uwepo wa fasihi simulizi ya zamani na kwa upande mmoja, fasihi simulizi mpya (ya sasa), na hata kwa upande mwingine uwepo wa fikra za fasihi simulizi ijayo. Mawazo haya yamekuwepo na yamejengwa katika fasihi na kumbukumbu zetu tangu mwanzo, kwamba kama kuna jambo lililotendwa jana, basi lipo jambo jingine ambalo litatendwa leo (ambalo litakuwa bora kuliko lile la jana) na vivyo hivyo lipo jingine ambalo linakusudiwa kutendwa kesho na ambalo litakuwa bora kuliko la jana. Kwa uhalali huo basi, fasihi simulizi twaweza kuigawanya katika makundi yafananayo na hayo, ambayo ni fasihi simulizi ya zamani, fasihi simulizi ya kileo (kisasa) na fasihi simulizi ijayo. Fasihi simulizi mpya ambayo ni ya kisasa ndiyo fasihi simulizi yenye kubeba dhana ya teknolojia mpya. Aidha ni vigumu kubashiri ya kuwa fasihi simulizi ijayo itajishughulisha na mambo

gani bila kuwashirikisha wataalamu wa taaluma husika. Wataalamu wa nyota, wanajimu na watabiri wanajitahidi kwa kiasi kikubwa kutuonyesha kuwepo kwa fasihi simulizi hii.

Kwa vile lengo la makala haya ni kuangalia kwa undani simulizi iliyoletwa katika fasihi na teknolojia mpya, makala yataangalia dhima ya fasihi hii katika jamii ambapo kuna fasihi ya kileo tendwa mf. Muziki wa kileo na mitambo ya kielektroniki (Televisheni, Video na Intaneti). Simulizi hizi zilianza kuonekana katika fasihi simulizi mapema katika karne ya ishirini, lakini zilionesha kushamiri zaidi katika ulimwengu wa kileo katika ulimwengu wa tatu mwishoni mwa karne ya ishirini na mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja.

2. Maana ya fasihi simulizi

Fasihi simulizi imeelezwa kwa namna tofauti na wataalamu mbalimbali wa fasihi.

Kirumbi (1975:15) ameona kwamba, fasihi simulizi ni masimulizi tunayoyapokea mdomo kwa mdomo, si masimulizi yaliyoandikwa tangu awali, kwa ajili hii basi, tutaona katika fasihi simulizi kuna utumiaji wa ulumbi (ufundi wa kusema).

Matteru (1983:26) anatueleza kuwa fasihi simulizi ni aina ya fasihi ambayo hutumia mdomo kwa kuumbwa, kuwasilishwa na kusambazwa kwa wasikilizaji na watumiaji wake. Aidha Matteru anaendelea kusema kwamba, fasihi simulizi ikiwa ni sanaa itumiayo maneno katika kutoa dhana fulani, hutegemea sana nyenzo mbalimbali za kuonekana na kusikika zitumiwazo na binadamu katika kujieleza.

Msokile (1992:3) anafafanua kwamba fasihi simulizi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha. Kazi hii huhifadhiwa kwa kichwa na kusambazwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo. Anamalizia kwa kusema kwamba, fasihi simulizi imekuwa ikirithishwa kutoka kizazi hadi kizazi.

Mlacha (1995:16) ametueleza kwamba fasihi simulizi ni nyanja katika maisha ya jamii ambayo huchangia sana katika kuiendeleza na kuidumisha historia ya jamii husika. Alipokuwa akifafanua zaidi juu ya fasihi simulizi Mlacha alisema kuwa ‘fasihi simulizi huchangia katika kuelimisha jamii kuhusu asili yake, chanzo na maendeleo ya utamaduni wake na maisha ya jamii hiyo kuanzia zamani’.

Wamitila (2003:44) anatueleza kwamba, fasihi simulizi ni dhana inayotumika kurejelea kazi ambazo kimsingi hupokezanwa kwa njia ya masimulizi au kwa mdomo. Yeye kwa hakika hayuko mbali sana na msingi mkuu wa fasihi simulizi uliosababisha kuwepo kwa tawi hili la fasihi. Kwa upande mwingine Wamitila (2003:15) anatueleza kuwa tawi hili la fasihi linatumiwa katika jamii kama njia ya kupashana maarifa yanayohusu utamaduni fulani, historia ya jamii, matamanio yao, mtazamo wao na historia yao. Kwa mtazamo wake huo, tunaweza kujumuisha kuwa fasihi simulizi ndicho chombo muhimu cha jamii.

Mwanafasihi Kimani Njogu (2006: 2) anatueleza kuwa fasihi simulizi ina ubunifu na uhai wa kipekee wenye kutoa fursa njema ya kuibua nadharia za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Pia anaifananisha aina hii ya fasihi na uti wa mgongo wa maendeleo ya binadamu, kwani ndani yake kuna masimulizi, maigizo, tathmini za mazingira na mahusiano ya kijamii.

Kwa mawazo ya wataalamu hawa, twaweza kuhitimisha ya kuwa fasihi simulizi ni sanaa inayotumia lugha ya mazungumzo ya ana kwa ana katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira husika. Hii ni sanaa ambayo ujumbe wake upo katika mfumo mzima wa pande mbili za mawasiliano kuwepo pamoja ana kwa ana hii ikimaanisha fanani yaani mtu anayerithisha (msimuliaji) na Hadhira yaani mtu anayerithishwa (msimuliwaji). Kwa njia hii fasihi simulizi hushirikisha au huwafikia watu wengi na mawazo ambayo jamii iliyakubali, imeyakubali, inaendelea kuyakubali yatokeapo na inayapitisha na au kuyakabidhi kwa kuendelezwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine kwa njia ya mdomo. Kwa hali hiyo basi, kwa vile taarifa zinazopatikana ni za mdomo, upo uwezekano wa utata, upotoshwaji na upoteaji wa taarifa muhimu za kale ambazo kama zingeliandikwa zingelidhihirisha ukweli wa mambo yalivyokuwa. Haiyumkini mapokeo ya fasihi simulizi yanachangia kwa kiasi kikubwa katika kuiunda, kuirekebisha, kuifundisha na kuiboresha jamii.

Fasihi simulizi ndiyo fasihi ya awali. Aina hii ya fasihi imeanza wakati binadamu alipoanza kutumia lugha kama moja ya chombo cha mawasiliano. Tangia hapo ndipo mwanadamu alipoanza kuimba, kutumia methali, vitendawili, nahau, n.k.

Jinsi dunia ilivyobadilika kimaendeleo, na fani za fasihi simulizi ziliendelea kubadilika. Kutokana na mabadiliko hayo ya binadamu tangu alipomudu kutumia lugha, uwepo wa maendeleo endelevu hadi kutokea kwa mapinduzi ya viwanda na baadaye mwishoni kuingia kwa teknolojia mpya, haya yote yalisababisha mabadiliko hadi katika fasihi simulizi. Mabadiliko haya yaliigawa fasihi simulizi katika *fasihi simulizi ya zamani* ambapo ilianza sambamba na binadamu kujua kutumia lugha. Baada hapo, kulipotokea maendeleo ya mitambo na kutokea mapinduzi ya viwanda, pakatokea mabadiliko katika fasihi simulizi na kukatokea *fasihi simulizi ya kisasa*. Kuingia kwa teknolojia mpya kuliibadili fasihi simulizi ya sasa, hivyo kuanzia sasa twaweza kuipa jina la *fasihi simulizi teknolojia mpya*. Kwa nadharia hiyo basi, makala haya yataangalia aina kuu mbili tu za fasihi simulizi yaani fasihi simulizi ya zamani na ile ambayo kwa mapokeo ya kisasa ni ya fasihi simulizi teknolojia mpya.

2.1 Fasihi simulizi ya zamani

Fasihi simulizi ya zamani ilikuwa ni sanaa ambayo imejengwa katika mfumo uliozoeleka wa kufikisha ujumbe kwa hadhira, mfumo uliolenga zaidi katika kurithishana mila, desturi na tamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hii ina maana kurithishana mila, desturi na tamaduni kutoka kizazi cha kale (babu, bibi na wengineo wa umri wao) kwa kukifundisha kwa kukirithisha kizazi kipya (ambacho ni watoto na wajukuu zao). Katika utoaji wa sanaa hii ni lazima pande zote mbili ziwepo.

Fasihi hii ilirithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine kupitia katika nyimbo, hadithi, ngoma, mashairi ya zamani (malenga), na hata michezo ya ujasiri na majigambo.

Katika kuiwasilisha fasihi hii ni lazima kuwepo na pande mbili za mawasiliano (majadiliano) yaani Fanani (anayerithisha, msimuliaji) na Hadhira (anayerithishwa, msimuliwaji). Fanani hujitahidi kutumia mbinu mbalimbali kuijenga kazi yake ili iweze kuvutia hadhira. Uhusiano

wake hujitokeza anapotumia viungo vyake vya mwili katika kujenga kazi yake. Lengo la fanani kutumia viungo hivyo ni kuwa anataka kuyakamilisha maadili yatokanayo na kazi yake. Msimuliaji anapochukua nafasi ya wahusika, mfano endapo kuna wimbo ndani ya hadithi na makofi, au ishara fulani ya kutumia viungo vya mwili; msimuliaji anapoimba na kupiga makofi, hapo anakuwa msimuliaji wa wakati huohuo pia ni mhusika mshiriki. Lazima ikumbukwe kwamba, fanani siku zote huanzisha majadiliano au mafundisho na Hadhira lazima iwe na uwezo wa kupokea na kuihifadhi majadiliano au mafundisho.

Fasihi simulizi ya zamani ilikuwa ikihifadhiwa kichwani. Ilihifadhiwa humo kwa muda mrefu kiasi kwamba baada ya muda ilibidi ipatiwe kizazi kingine na kingine. Ingawaje katika kukipatia kizazi kingine yale yaliyokuwapo sio yote ambayo yalifikishwa kwa kizazi kipya, bali yaliyofikishwa yalikiwezesha kizazi kipya kufahamu yaliyotokea na kutendeka hapo zamani. Fasihi hii ilikuwa haijaathirika kwa maana kwamba kipindi chote hicho tamaduni asilia zilikuwa hazijaingiliwa na tamaduni za kigeni zenye nguvu. Hivyo basi, mmiliki wa fasihi simulizi katika kipindi na wakati huo alikuwa ni mwana jamii na fasihi hii ilikuwa ni mali ya jamii. Fasihi simulizi ya zamani ilikuwa na mvuto wa aina yake, ambapo kukosea au kwenda kinyume na maadili ya jamii ilikuwa si rahisi kwa sababu jamii ilikuwa pamoja kwa muda mwingi.

Baada ya mwingilio wa wageni toka pande mbalimbali za dunia, fasihi simulizi ilianza kubadilika kutokana na kuingizwa kwa mila, desturi na tamaduni toka kwa wageni hawa. Ama kwa hakika wageni hawa walifanikiwa kwa kiasi kikubwa kuathiri fasihi simulizi na kuipa mkondo mpya. Jamii iliyapokea mafanikio ya wakoloni yaliyodhihirika wakati wanajamii wenyewe walipoamini kwamba amali walizokuwa nazo hazikuwa na maana kama zile walizoletewa na wageni au wakoloni hawa. Jamii iliamini kwamba amali hizo hawakuwa nazo, na kama walikuwa nazo, basi hazikuwa na maana kama zile walizoletewa. Kwa mfano wakati jamii ilifurahia kuburudishwa na kuburudika kwa kutumia simulizi zilizotolewa jioni kwa pamoja mbele ya nuru ya mbalamwezi, kuingia kwa wageni hawa kumesababisha kuwepo kwa fasihi simulizi nyingine ambayo kwa kiasi kikubwa kumeadhiri starehe hiyo. Kadhalika wageni hawa wamechangia sana kuingia kwa maendeleo ya kisayansi na teknolojia ambayo yameanza kuiingiza jamii yetu katika fasihi ya televisheni, kompyuta redio na video ambayo kwa kiasi kikubwa imefifisha starehe iliyokuwa ikipatikana hapo awali. Amali hizi mpya kama televisheni, kompyuta, redio na video ndizo zinazotumika kuiwasilisha fasihi simulizi ya kisasa na ambazo tutaziangalia uwepo wake na athari zake katika jamii.

2.2 Fasihi simulizi teknolojia mpya

Tunapozungumzia juu ya Teknolojia ni lazima tuhusishe na Sayansi, ambapo tunapozungumzia juu ya teknolojia tunayazungumzia maendeleo ya Kisayansi. Kwa hivyo basi Sayansi na Teknolojia ni vitu viwili vinavyokwenda sambamba na pamoja bila ya kuachana. Bali, teknolojia ni maendeleo ya kisayansi katika hatua ya mwisho kabisa ambayo inaonekana. Historia inaonyesha kwamba nchi zote ambazo zimeendelea, maendeleo yake yametokana na Sayansi na Teknolojia.

Tunatumia teknolojia katika maisha yetu ya kila siku; mfano nyumba, mawasiliano, mwanga n.k. Halikadhalika tunatumia teknolojia kwa matumizi mengi ya kila siku, kupikia, kuwasiliana, kutembeleana na mambo mengine yanayofanana na hayo.

Tunapozungumzia juu ya Teknolojia mpya, tunamaanisha maendeleo zaidi katika Sayansi na Teknolojia. Na tunapozungumzia juu ya fasihi simulizi teknolojia mpya, tunazungumzia jinsi ambavyo tunaweza kuitumia Teknolojia mpya katika kuihifadhi, kuiwakilisha, kuikosoa, kuburudisha na hata kuichangia mada fasihi simulizi. Na hayo yote yanawezekana kupitia televisheni, kompyuta, mikanda ya video, mikanda ya CD, barua pepe, simu za mkononi, setelaiti n.k. Labda hapa niweke wazi ya kuwa nitakachokieleza manufaa ya teknolojia mpya kwa fasihi simulizi na kwa jamii nzima kwa ujumla.

Kwanza, katika kuiwakilisha fasihi simulizi kwa watu wengi waliombali na fanani, kwani hii ni fasihi ambayo uwasilishaji wake si lazima wahusika wote wawili wawepo yaani fanani na Hadhira. Hadhira inaweza kuwepo lakini fanani asiwepo na nafasi yake ikachukuliwa na utaalamu wa kisasa unaotokana na teknolojia mpya. Hili hufanyika kupitia mikanda ya video na ya CD, kupitia kompyuta, barua pepe, radio, setelaiti n.k. Kwa ujumla hapa teknolojia mpya inatumika kama kihifadhi cha fasihi simulizi ili kuweza kufikisha ujumbe.

Pili, katika kuihifadhi fasihi simulizi ili vizazi vingine viweze kuirithi, nyanja hii ya fasihi hutumia vyombo vya kisasa kabisa vya kuhifadhia kama mikanda ya video, DVD, tepurekoda na utepe wake, kompyuta, CD n.k.

Tatu, katika kuchangia mada, teknolojia mpya inatumika kama kiunganishi kati ya fanani na hadhira, ambapo mfano mzuri katika eneo hili ni matumizi ya setelaiti. Aidha setelaiti yaweza kutumika kuiwasilisha kazi ya fasihi simulizi kwa hadhira iliyo mbali na fanani kama alivyofanya aliyekuwa raisi wa Marekani Bill Clinton alipokuwa akichangia mawazo yake ili kuwezesha kupatikana kwa suluhisho la mgogoro baina ya nchi za Rwanda na Burundi. Raisi huyu alichangia moja kwa moja akiwa Marekani wakati mkutano wa suluhu ulikua ukifanyikia Arusha. Rais huyu alionekana kwenye setelaiti akizungumzia mtazamo wake kuhusu mgogoro huo.

Nne, katika kukosoa hii hufanyika kupitia televisheni, video hasa kwenye michezo ya kuigiza (Tamthilia) kupitia video na televisheni wasanii huikosoa jamii pale inapokuwa aidha imekosea au imepotoka, hivyo jamii inapata mafunzo kupitia teknolojia mpya. Tamthilia inaweza kuwa inachezwa na watu kutoka nchi nyingine kwa mfano Nigeria, lakini kwa kuwa matatizo ya kijamii hufanana basi mchezo huo unaweza kutoa mafunzo kwa jamii mbalimbali Duniani.

Tano, katika kuburudisha, hapa jamii inaburudishwa na vipindi mbalimbali vya kijamii katika tamthilia, muziki ngoma n.k. kupitia televisheni, video, kompyuta, DVD n.k.

Aidha kwa upande mwingine mabadiliko haya ambayo yameigeuza dunia kuwa ndogo na ndogo kila kukicha, yameonesha kwamba Udogo huu wa dunia unaotokana na teknolojia mpya ya mawasiliano, ambayo imekuwa ya kisasa zaidi. Teknolojia hii ndio iliyozaa dhana mpya ya fasihi simulizi ya kileo iliyochukua nafasi ya dhana iliyoitangulia ya fasihi simulizi

ya zamani. Kwa mtazamo wa juu zaidi twaweza kusema kuwa ni fasihi ambayo watu wa kizazi hiki wanaiita kuwa ni fasihi inayokwenda na wakati, fasihi ya kisasa au fasihi iliyokwenda shule.

Wataalamu wengi wa intaneti wamefungua tovuti mama kwa nia ya kuharakisha mawasiliano duniani. Wanafunzi wengi sana wamejifunza kutumia kompyuta na kwa kupitia teknolojia hii wamekuwa wakipata elimu ya mbali kwa gharama nafuu. Teknolojia ya setelaiti, intaneti imekuwa ikitumika ili kuboresha elimu ya juu na kupiga hatua ya maendeleo ya sayansi na teknolojia. Aidha televisheni, video, mitambo ya setelaiti na ving'amuzi vimekuwa vikitoa misaada inayojumuisha mafunzo makini ya kuwasaidia walimu kuboresha taaluma zao. Walimu na wanafunzi waliokuwa katika hali ya kukata tamaa juu ya namna ya kuimarisha ufundishaji, wameanza kubaini matunda ya mpango huu wa kutoa elimu kwa kutumia teknolojia hii. Japokuwa katika mpango huu vifaa ni haba, shule na vyuo vinaendelea kujitahidi kuongeza ufanisi wa ufundishaji wake pamoja na kuimarisha jamii watokako wasomaji. Hatua hii hapana shaka itasaidia sana katika kuongeza viwango vya wanafunzi kufaulu.

Kwa upande mwingine tumeona kwamba maendeleo haya ya programu za kompyuta yameikuza elimu ya sayansi na teknolojia kwa kiasi kwamba hata madaktari bingwa wa upasuaji wa magonjwa ya moyo wamekiri kuwa inafaa. Aidha kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na mwandishi wa gazeti la Mtanzania la tarehe 13.06.03 ukurasa wa 9 ambapo mwandishi ambaye jina lake halikutajwa aliinukuu makala iliyochapishwa katika gazeti la Uingereza *Sunday Times* Kwa mujibu wa makala hiyo, mwandishi ametuelezea jinsi elimu ya sayansi na teknolojia inavyotufikisha mbali akiwa anatumia mfano wa programu ya kompyuta iliyovumbuliwa na wataalamu huko Uingereza inayoweza kuwaamba mabingwa wa upasuaji iwapo inafaa kumfanyia upasuaji mgonjwa wa moyo.

Hapa wataalamu wamejitahidi kutuonyesha namna teknolojia mpya hii ilivyopiga hatua hadi kuweza kuaminika katika upasuaji wa sehemu hii muhimu kabisa katika mwili wa binadamu, ulinganifu kati ya gharama za matibabu ya mgonjwa na urefu wa manufaa atakayoyapata kiafya.

Kwa kuangalia maendeleo hayo ya kasi ya teknolojia ya mawasiliano na kuzingatia ukweli uliojitokeza kwamba dunia ni mahali pa ujirani, kuna aina fulani ya kukaribiana kwa watu kupitia hizo njia mpya na za kisasa zaidi za mawasiliano.

Kama tulivyokwishaona, hivi sasa dunia hususan, nchi za dunia ya tatu tumeikubali kwa hiari yetu wenyewe na kuipokea aina hii mpya ya fasihi simulizi. Aidha katika kuikubali huku, kumetokea na kumekuwepo na vituo vingi vya mitandao ya kielektroniki ambapo vijana wanapoteza muda mwingi sana kuwasiliana na vijana wenzao duniani, wanabadilishana mawazo na kuelimishana mambo mengi sana yanayowahusu vijana hao.

3. Athari za uwepo wa teknolojia mpya katika fasihi

Hakuna jambo zuri linalotokea duniani bila ya kupatikana kwa ubaya wake. Mafanikio haya ya kisayansi na teknolojia mpya, yameleta athari kubwa sana katika fasihi simulizi, hususan

katika utamaduni, mila na desturi zetu. Amali hii ambayo ni utajiri mkubwa wa taifa lolote lile ni muhimu sana katika nchi.

Teknolojia mpya ni utamaduni mpya kutoka nchi za Ulaya na Marekani zilizoendelea, ambazo zina utamaduni wenye nguvu ukilinganisha na tamaduni za Kiafrika ambazo ni dhaifu kimataifa. Kwa hivyo, kutokana na Utandawazi tunalazimika kuonyesha vipindi vingi vya Tamthilia vya nje ya nchi kuliko vya ndani ya nchi. Mfano tamthilia nyingi za kigeni kama *Egoli*, *The Bold & The Beautiful*, *Days of Our Life*, *La Mujer de mi Vida* (*Woman of My Life*), *Isindingo*, n.k. zinaonyeshwa na Televisheni zetu za hapa nyumbani kama ITV, TVT, STAR TV, DTV, Channel Ten n.k.

Teknolojia mpya inaenda sambamba na Utandawazi ambao ndani yake kuna udhalilishwaji wa nchi za ulimwengu wa tatu kama Tanzania. Kwa hali hiyo utakuta kuwa nafasi ya fasihi simulizi ya nchi zinazoendelea kama Tanzania katika teknolojia ni finyu sana katika kujitangaza.

Matumizi ya zana za kisasa katika muziki wa dansi, hususan Bongo Flava yanachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza ladha halisi ya kitamaduni ambayo ingepatikana kama ngoma, marimba, vinubi, matoazi na ala nyingine zingetumika. Aidha kwa kutumia fasihi simulizi ya kileo kumezuka lugha za namna nyingi katika jamii zetu. Lugha hizi zimetokana aidha na filamu jamii inazoziangalia katika vipindi vyetu vya televisheni. Kumekuwepo na misuguano kadhaa kati ya watu wa bara na watu wa pwani hususan wa Dar Es Salaam kuhusu lugha za mitaani zinazotumika katika televisheni zetu ambazo watanzania wenzao wa Bara wanashindwa kukubali kwani baadhi ya misamiati hiyo haipo katika misamiati ya Watanzania wenzao. Kwa mfano msamiati anaoutumia msanii Bambo: *kukuruku mwanagu, Aluu, Urodu n.k.* au msamiati anaoutumia mzee Jongo na wengine wengi.

Halikadhalika kumekuwa na wimbi kubwa la wanajamii pamoja na mashabiki wanaoshabikia filamu na maonyesho mengi yanayoonyeshwa katika televisheni na kumbi zetu za starehe. Filamu hizi na maonyesho haya yanatuonyesha mila, desturi na itikadi za jamii husika. Kwa mfano onyesho lililomalizika la *The Big Brother Africa*, Filamu za *Isidingo*, *Passion*, *The Bold & the Beautiful*, na nyinginezo nyingi za Kimarekani, Kinaijiria, Kighana, Kikongo, Kihindi na nyinginezo nyingi. Mapokeo ya filamu hizi kwa jamii ya Kitanzania ni yale ya kupata na kujua tamaduni za wenzetu hawa. Katika kupata na kuiga tamaduni hizo za wenzetu, ni dhahiri kwamba kunabadilisha mwenendo na mwelekeo wa taifa kisiasa, kijamii, kiutamaduni, kisaikolojia na kiitikadi. Mabadiliko haya yanaweza kuibadilisha jamii hususan vijana wa marika yote katika kuiga tamaduni, mila na desturi za mataifa mbalimbali.

Aidha maneno yanayotumika katika nyimbo zinazoimbwa na wasanii wanaoshiriki kucheza filamu mbalimbali hayasikiki vizuri, lugha wanayoitumia haiendani na maadili ya mila na desturi za Kitanzania. Nyimbo nyingine hazina mafunzo mazuri katika muktadha wa jamii ya Tanzania. Wengi wa wanamuziki wanajitangazia tu umaarufu wao pasipokujua kuwa wanatakiwa kuutangaza utamaduni wa Kiafrika. Midundo wanayoipiga na mitindo wanayoicheza haionyeshi utamaduni wa Mwafrika bali inamdhalilisha Mwafrika kwa kuonyesha namna jin-

sia moja inavyodhalilishwa. Hii ina maana kwamba mdhalilishwaji wa kwanza katika nyimbo, filamu au maigizo tunayoyaonyeshwa aidha katika luninga zetu au tunazozisikia katika vipindi vya redio daima ni mwanamke. Zaidi ya hayo, yote tusikiayo na tuonyeshwayo yanalengwa katika utamaduni wa magharibi zaidi kuliko utamaduni wa Kitanzania au wa Kiafrika kwa ujumla. Matamasha yanayotumiwa na wasanii wetu sio yale ya kuinua vipaji vyao kisanii bali ni ya kuiga mila na desturi za Mataifa ya wenzetu na wala sio za kwetu. Hii imewasababisha wasanii wengi kudumaa na kuona kuwa hakuna haja ya kubuni na kujifunza dhana nyingine

Fasihi simulizi ya kileo si mali ya jamii. Hii ni mali ya wachache kwani inapotolewa kupitia vikundi vya sanaa na utamaduni ni lazima watu walipe ili waweze kuishuhudia. Kwa hiyo imekuwa ni biashara kuliko hali halisi.

3.1 Faida za uwepo wa teknolojia mpya katika fasihi

Teknolojia mpya ni njia ya kisasa zaidi katika kuhifadhi fasihi simulizi ili kutunza kumbukumbu. Kwa mfano historia ya zamani ya Tanzania kabla ya ukoloni kuhusu maisha ya mababu na mabibi zetu inaweza ikarekodiwa kwenye mikanda na kusikilizwa na hadhira.

Kwa utashi huo ina maana kuwa teknolojia mpya ni utaalamu wa hali ya juu, hivyo kazi zimekuwa za ubora wa hali ya juu. Teknolojia mpya ina faida nyingine nyingi katika kukuza fasihi simulizi ya Kiswahili. Mfano katika Tanzania ya leo tuna vituo vingi vya redio na televisheni ambavyo hurusha matangazo yake sehemu mbalimbali hapa nchini. Kwa kupitia vituo hivi fasihi simulizi imeweza kuwafikia watu wengi ambao wako mbali ambako matangazo hayo ya redio na televisheni yanafika. Katika vituo mbalimbali vya televisheni hapa nchini kuna vipindi mbalimbali vya watoto ambapo hadithi, vitendawili, methali, mafumbo husimuliwa kwa watoto walioko pale studio na wengineo ambao huyapata matangazo hayo kupitia sehemu walizopo. Katika televisheni ya ITV kuna kipindi cha watoto kila siku ya Jumapili saa tatu asubuhi. Vilevile katika televisheni hiyohiyo siku ya Jumapili saa tisa alasiri kuna kipindi cha mgongano wa mawazo ambapo fasihi ya Kiswahili ya Mtanzania husimuliwa kwa jamii hasa fasihi ya vitabu ambapo huwa kuna mjadala kuhusu mada mbalimbali za kifasihi na huendeshwa na wanafunzi chini ya usimamizi wa walimu wao.

Kwa upande wa redio vipo vipindi kadhaa katika Radio One Stereo, ambapo baadhi yake ni kile cha watoto ambacho hurushwa kila siku ya Jumamosi asubuhi, na kimekwishadumu kwa muda mrefu kikiwa kikiendeshwa na mtangazaji wa siku nyingi wa redio hapa nchini Julius Nyaisanga, ambaye katika kipindi hicho cha watoto hujulikana kama babu wa kimanzichana. Kimanzichana ni moja ya sehemu maarufu katika mkoa wa Pwani ambayo ipo kijijini. Radio Tanzania na Televisheni ya Taifa nao hawako nyuma katika hilo. Nao pia wana vipindi mbalimbali kama zilivyo redio na televisheni nyingine. Mfano mzuri redio Tanzania wana vipindi kama cheichei shangazi na mama na mwana, ambapo hadithi mbalimbali zenye semi, mafumbo, methali na vitendawili husimuliwa.

4. Hitimisho

Fasihi simulizi ya zamani ilikuwa imekitwa katika misingi mikuu miwili; moja, mila na desturi. Mbili, fasihi simulizi ya kale ililenga kutoa huduma zaidi na si biashara. Fasihi hii inafikisha ujumbe katika jamii ikiwa na lengo la kuelimisha, kuonya, kuburudisha na kukosoa.

Teknolojia mpya katika fasihi simulizi ina faida na hasara kama tulivyobainisha. Fasihi simulizi hii imekitwa katika misingi mikuu miwili. Moja, sayansi na teknolojia; mbili, ni biashara. Fasihi hii inaua utamaduni wa Kitanzania. Mfano watoto na vijana wengi hivi sasa wanafurahia na kufahamu mambo mengi ya Ulaya, Amerika na tamaduni zao kuliko tamaduni za Tanzania. Haya wanayafahamu kupitia televisheni, video na internet. Fasihi simulizi ya kileo imekuwa ni biashara zaidi kuliko kutoa elimu kwa jamii kama huduma ya kawaida. Hivyo kwa kadri tunavyozidi kuwa karibu zaidi utandawazi na matumizi ya teknolojia mpya katika maisha yetu ya kila siku, nchi za Kiafrika ni lazima ziwe bunifu kwa tamaduni zao wenyewe ili kuepukana na hasara zinazopatikana kutokana na kuwepo kwa teknolojia mpya.

Aidha kwa upande wa vifaa, nchi nyingi za Kiafrika zimeshindwa kuagiza vifaa na kutumia teknolojia mpya kutokana na sababu kwamba ni ghali sana. Hii inahatarisha uchumi wa nchi hizi kwa kuzifanya ziwe tegemezi katika kuipata teknolojia mpya. Teknolojia mpya ni nguzo muhimu sana katika maendeleo ya fasihi simulizi si katika Tanzania tu, bali ulimwenguni kwa ujumla. Hii ni kwa sababu inawawezesha watu wengi zaidi kupata matangazo ya moja kwa na wakati mwingine wao kushiriki kwa kupiga simu na kuchangia wanachopaswa kama ni kusimulia hadithi, vitendawili, nyimbo, ngonjera n.k. Lakini wengi wanaofaidi huduma hii ni wale walioko mijini na katika vijiji vichache ambapo matangazo ya redio na televisheni yanafika na kwa bahati nzuri katika Tanzania ya leo sehemu nyingi sana za mijini na vijijini wanapata matangazo ya redio mbalimbali zilizopo nchini. Kwa upande wa televisheni zaidi ni mijini kuliko vijijini ndio wanao faidi huduma hii. Teknolojia mpya ina faida nyingine nyingi katika kukuza fasihi simulizi ya Kiswahili. Mfano katika Tanzania ya leo tuna vituo vingi vya redio na televisheni ambavyo hurusha matangazo yake sehemu mbalimbali nchini. Kupitia vituo hivi fasihi simulizi imeweza kuwafikia watu wengi ambao wako mbali ambako matangazo hayo ya redio na televisheni yanawafikia.

Katika vituo mbalimbali vya televisheni hapa nchini kuna vipindi mbalimbali vya watoto ambapo hadithi, vitendawili, methali, mafumbo husimuliwa kwa watoto walioko pale studio na wengineo ambao huyapata matangazo hayo kupitia sehemu walizopo. Katika televisheni ya ITV kuna kipindi cha watoto kila siku ya Jumapili saa tatu asubuhi. Vilevile katika televisheni hiyohiyo siku ya Jumapili saa tisa alasiri kuna kipindi cha mgongano wa mawazo ambapo fasihi ya Kiswahili ya Mtanzania husimuliwa kwa jamii hasa fasihi ya vitabu ambapo huwa kuna mjadala kuhusu mada mbalimbali za kifasihi na huendeshwa na wanafunzi chini ya usimamizi wa walimu wao. Kwa upande wa redio katika Radio One Stereo kuna kipindi cha watoto kila siku ya Jumamosi asubuhi ambacho kwa muda mrefu kimekuwa kikienendeshwa na mtangazaji wa siku nyingi wa redio hapa nchini Julius Nyaisanga, ambaye katika kipindi hicho cha watoto hujulikana kama babu wa kimanzichana. Kimanzichana ni moja ya sehemu

maarufu katika mkoa wa pwani ambayo ipo kijijini. Radio Tanzania na Televisheni ya Taifa nao hawako nyuma katika hilo. Nao pia wana vipindi mbalimbali kama zilivyo redio na televisheni nyingine. Mfano mzuri redio Tanzania wana vipindi kama cheichei shangazi na mama na mwana, ambapo hadithi mbalimbali, mafumbo, methali na vitendawili husimuliwa.

Marejeo

Gazeti la Mtanzania la tarehe 13.06.03.

Kimani N. 2006. Fasihi Simulizi na Nadharia ya Fasihi ya Kiafrika, katika *Fasihi ya Kiswahili*. Nairobi: Twaweza Communications. Uk. 1 – 10.

Kirumbi, P. S. 1975. *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Shungwaya Publishers.

Matteru, M. D. 1983. Fasihi Simulizi na Uandishi wa Kiswahili, katika Fasihi: *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI. Uk. 26 – 37.

Mlacha, S. A. K. 1995. Fasihi Simulizi na Usuli wa Historia ya Pemba. Katika: *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI/ITAA. Uk. 16-26.

Msokile, M. 1992. *Kunga za Fasihi na Lugha*. Kibaha: EPD.

Wamitila K. W. 2003. *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi, Kenya: Focus Publications.

Wamitila, K. W. 2003. *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Fasihi*. Nairobi, Kenya: Focus Publications.